# TANGAZO KWA UMMA

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

## TANGAZO LA MIKOPO KWA VIJANA AWAMU YA PILI

Katika kutekeleza ahadi ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kutoa shilingi bilioni 200 kwa vijana ndani ya siku 100 baada ya kuingia madarakani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inautangazia umma kuanza kwa Awamu ya Pili ya utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana.

Malengo ya mikopo hiyo ni kuwawezesha vijana kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza biashara ndogo, biashara za kati na kampuni changa ili kujiajiri kupitia Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mikopo hiyo itatolewa kwa njia ya vifaa na pembejeo za uzalishaji, ikiwemo ufugaji wa samaki kwa vizimba, ufugaji wa kuku (chotara, mayai na nyama), mbuzi, kondoo na nguruwe, pamoja na boti za kuhudumia vizimba, boti za uvuvi, zana za uvuvi, mifumo ya ubaridi (cold chain) katika mazao ya uvuvi, mifumo ya kuzalisha vifaranga vya samaki, mifumo na vifaa vya uchakataji wa mazao ya uvuvi ikijumuisha makausho ya dagaa na mwani (*dryers*).

Vigezo na maelekezo kwa waombaji ni kama ifuatavyo:

i. Barua ya maombi na fomu ya maombi iliyojazwa;
ii. Awe na umri kati ya **miaka 18 hadi 35**;
iii. Awe mkazi wa eneo utakapofanyika mradi husika na awe na barua ya uthibitisho kutoka kwa Mtendaji wa Serikali za Mitaa/Vijiji;
iv. Awe na uthibitisho wa kuwa raia wa Tanzania (Kitambulisho cha Taifa - NIDA, au Namba ya NIDA, kadi ya mpiga kura, leseni ya udereva, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria);
v. Mwombaji anaweza kuomba kama mtu binafsi, kampuni ya vijana, Chama cha ushirika, au kikundi kilichosajiliwa na Halmashauri husika;
vi. Awe na barua na vitambulisho (NIDA) vya wadhamini wawili (2) wanaotambulika kwenye uongozi wa Serikali ambao watawajibika kulipa deni endapo mnufaika atakiuka masharti ya mkopo huu;

vii. Awe na andiko lenye kuelezea mahitaji ya **mradi kulingana na miradi iliyotajwa kwenye tangazo** hili;

viii. Asiwe na **mikopo chechefu** kutoka katika taasisi za fedha au taasisi yoyote nchini; na

ix. Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) kwa kampuni.

Inasisitizwa waombaji wawasilishe maombi yao yaliyokamilka kulingana na vigezo vilivyotolewa. Maombi yote yawasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kabla au ifikapo tarehe **14 Septemba, 2026**. Fomu ya maombi imeambatishwa. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia namba ya huduma kwa wateja **0737-476937.**

Imetolewa na;

KATIBU MKUU
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
Mji wa Serikali Mtumba,
S. L. P. 2870,
40487 DODOMA
Barua pepe: barua@mlf.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Affix recent coloured passport size photograph

# FOMU MAALUM KWA AJILI YA VIJANA KUOMBA MKOPO

## 1.0. MAELEZO

Fomu hii itajazwa na mwombaji binafsi au kiongozi wa kampuni, kikundi, au chama cha ushirika cha vijana kinachoomba mkopo. Viambatanisho vifuatavyo ni muhimu kwa ajili ya uhakiki wa mwombaji wa mkopo:

i. Barua ya maombi na fomu ya maombi iliyojazwa;
ii. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji wa Serikali za Mtaa/Kijiji;
iii. Nakala za utambulisho wa uraia wa mwombaji au viongozi wa kikundi, kampuni au chama cha ushirika. (Kitambulisho cha Taifa - NIDA, au Namba ya NIDA, Cheti cha kuzaliwa, Hati ya Kusafiria);
iv. Andiko la mradi lenye maelezo ya kwanini anahitaji mradi husika; cheti cha usajili wa kikundi, chama cha ushirika au kampuni;
v. Nakala ya Katiba ya Kikundi au Chama cha Ushirika au Hati ya makubaliano na kanuni za kampuni;
vi. Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) kwa kampuni;
vii. Barua na vitambulisho (NIDA) vya wadhamini wawili (2) wanaotambulika kwenye uongozi wa Serikali za Mtaa/Kijiji;
viii. Asiwe na mikopo mingine katika taasisi za fedha ambayo muombaji ameshindwa kuilipa; na
ix. Muktasari wa wanachama kukubaliana kukopa kwa vyama vya ushirika na vikundi.

## 2.0. Taarifa ya kikundi

i. Jina la mwombaji……………………………;
ii. Aina ya Mwombaji (Binafsi/kikundi/Chama /Kampuni)…………………………
iii. Majina ya Viongozi (kikundi/Chama /Kampuni) na namba za simu
   - ✓ M/Kiti: Jina…………………………....... Simu............................................
   - ✓ Katibu: Jina…......................................Simu .........................................
   - ✓ Mhazini (vikundi na vyama vya ushirika)/Mhasibu (Kampuni): Jina ...................................... Simu.......................................
iv. Idadi ya wanachama (kikundi/Chama /Kampuni)………Ke………Me…………
v. Anwani Kamili ..........................................................................

## 3.0 KWA AJILI YA MATUMIZI YA OFISI TU

Baaada ya tathmin wa maombi kubaini kama mwombaji anastahili/hastahili kupewa mkopo

A. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Halmashauri/Jiji/Mji/Manispaa/Wilaya
Jina la Afisa………………………….....…Cheo……………

Halmashauri ya …………………………. Sahihi………………… Tarehe…………...

Anastahili/hastahili kupewa mkopo:

Maoni/sababu ya maamuzi hayo:……………………........................……………
……...........................................................................................................................

B. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa.
Jina la Afisa……………………………………………Cheo…………………………
Mkoa ……………………………. Sahihi……………………… Tarehe………….
Anastahili/hastahili kupewa mkopo:

Maoni/sababu ya maamuzi hayo:……………………........................……………
……...........................................................................................................................

C. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi
Jina…………………………………Cheo………………………………………….
Idara……………………………Sahihi…………………. Tarehe………………….

Maoni……………………………...............…………………………………………